# NCHI NA URAIA
# HAKI NA WAJIBU KWA TAIFA

## الوطن والمواطنة

### الحقوق والواجبات


**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Muhammad A. Bahsan

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

ترجمة

# الوطن والمواطنة

## الحقوق والواجبات

تأ ليف

الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 2 7/31/2013 1:54:30 PM

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 - 17 - 028 - 9

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hasan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Muhammad A. Bahsan

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Desemba, 2013
Nakala: 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........................................................................ 01

Dibaji........................................................................................ 03

Utangulizi.................................................................................. 07

Nchi ni nini? Na Uraia ni nini ............................................................ 09

Kufukuzwa katika Nchi na Sheria ya Jihad ............................................. 14

Dini na kupenda Nchi yako................................................................. 18

Mipaka ya Nchi .............................................................................. 22

Wajibu wa Raia mbele ya Taifa lake..................................................... 26

Haki za Raia .................................................................................. 35



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 5 7/31/2013 1:54:31 PM

# NENO LA MCHAPISHAJI

N*chi na Uraia* ni kitabu chenye maudhui yanayohusiana na 'nchi, uraia, haki na wajibu kwa taifa.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa mihadhara ya Sheikh Hassan Musa al-Saffar aliyokuwa akiitoa nyakati mbalimbali na sehemu mbalimbali kwa ajili ya kuzungumzia mada mbalimbali kuhusiana na Uislamu, Waislamu na ubinadamu kwa ujumla.

Kama tunavyosema wakati wote kwamba Uislamu ni dini na mfumo kamili wa maisha; haukuacha lolote linalomhusu mwanadamu kimwili au kiroho na kuweka sheria ya kuyaendesha maisha hayo (kiroho na kimwili).

Katika kitabu hiki Sheikh anazungumzia suala la haki na wajibu wa raia katika taifa kwa mtazamo wa Kiislamu.

Sisi kama wachapishaji tunakiwasilisha kitabu hiki kama kilivyo kwa wasomaji wetu na kuwashauri wasome yaliyomo ndani yake, wayafanyie kazi na kuyazingatia na kufaidika na hazina iliyomo humo.

Hii ni moja kati ya kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwahudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa Kiswahili. Na kwa maana hiyohiyo, imeamua kukichapisha kitabu hiki chenye manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lilelile la kuwahudumia Waislamu hususan wanaozungumza Kiswahili.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 1 7/31/2013 1:54:31 PM

katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia na kugombanishwa wenyewe kwa wenyewe ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki Sheikh Hassan Musa al-Saffar kwa kazi  kubwa aliyofanya kwa ajili ya Umma huu wa Waislamu, Allah 'Azza wa Jallah amlipe kila la kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Halikadhalika tunamshukuru ndugu yetu Muhammad A. Bahsan kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah na yeye Allah 'Azza wa Jallah amlipe kila la kheri hapa duniani na Akhera pia, bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na huko Akhera.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation.**



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 2 7/31/2013 1:54:31 PM

# DIBAJI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

ٱلَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَـٰلَـٰتِ ٱللَّهِ وَيَخْشَوْنَهُۥ وَلَا يَخْشَوْنَ أَحَدًا
إِلَّا ٱللَّهَ ۗ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ حَسِيبًا ﴿٣٩﴾

**"Ambao walifikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwogopa Yeye, wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Ndiye anayetosha kuhisabu."** **(Al-Ahzaab 33:39)**.

Bado dhana nyingi na mambo mengi muhimu katika Uislamu hayafahamiki au hayafahamishwi vyema kwa mtu mmoja mmoja au jamii, bali yako mbali na hayafanyiwi hata utafiti makini, hali hii imesababisha hali ya kutokuwepo uoni sahihi kwa wale wanaojishughulisha na mambo yahusianayo na jamii au ya mtu mmoja mmoja katika mambo mazito yanayoihusu jamii.

Mazingatio ya Mwislamu huongezeka kutokana na kufikiri kwake sahihi na utekelezaji wake wa mafunzo ya Uislamu, na ubaya huzidi pale anapokwenda kinyume na mafunzo sahihi yaliyoletwa na Dini ya Kiislamu katika nyanja ya imani na sheria (matendo).

Kwa hivyo imekuwa ni lazima kusimama kwenye sehemu kubwa ya dhana hizi na mambo haya ili kuyatatua kwa upembuzi makini, na kuyasoma moja baada ya jingine katika nyanja zake zifahamikazo ili kuziba pengo hilo ambalo bado ni kikwazo kwa mtazamo wa Kiislamu, hasa katika hali tuliyonayo hivi sasa kwenye jamii.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 3 7/31/2013 1:54:31 PM

Hapana shaka kwamba umuhimu huu wa kuwazindua watu ni jukumu la wasomi na wanafikra wa Ummah wa Kiislamu, imekuwa ni jambo la wazi kwao, kwamba wanawajibika kufanya bidii katika kuondoa shaka na mkanganyiko katika fikra na mafundisho yasiyokuwa ya wazi ili kumzindua Mwislamu. Na kama vile ambavyo kila siku kunazuka fikra mpya katika maisha ya wanadamu, fikra ambazo huzalikana kutokana na maendeleo ya kielimu yanayojitokeza kwa kasi sana, inalazimu kuwepo utafiti wa kina katika kukabiliana na fikra hizo.

Ndio maana walikuwapo na wanaendelea kuwepo baadhi ya watu wema wa Ummah huu ambao wamejibebesha majukumu ya kufanya kazi kwa bidii zote ili kuwaamsha na kuwazindua watu kwa kuwapa maelekezo ya Kiislamu, kwa lengo la kumfanya Mwislamu katika pande zote za kijamii kuwa mwanaharakati mchapakazi mwenye kusimamia majukumu yake kwa ukamilifu na umakini.

Na katika hao wachache ambao wametoa juhudi zao na wanaendelea kutoa juhudi zao katika njia hii ni mwanachuoni maarufu; Ustadhi Sheikh Hassan Saffar ambaye hana haja ya kutambulishwa, yeye ni miongoni mwa wanaharakati wenye kuhubiri mafunzo na mwamsho mpya wa Kiislamu wenye kutoa dhamana ya kufikia njia ya mafanikio.

Na utafiti huu ulioko mbele yetu ni miongoni mwa lulu za mwanachuoni huyo, aliyetoa juhudi zake zote katika kunyanyua na kuutukuza Uislamu na watu wake. Mtu huyo ni mhubiri mzuri aliye makini, ambaye mimbari za kutolea hotuba zinamfahamu vyema kutokana na hotuba zake za kipekee, na kutokana na uzoefu wake juu ya mimbari kwa muda mrefu, amesaidia katika kuendeleza hali ya hotuba za mimbari na kufikia kuwa za kisasa zaidi, na kuegemea katika upekuzi na utafiti katika mambo na fikra mbalimbali, na amezama zaidi pale alipotabikisha njia, kanuni na misingi ya kielimu katika mahubiri yake.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 4 7/31/2013 1:54:31 PM

Lakini juhudi zake zote hizi hazikuweza kumsimamisha na kumzuia kuandika vitabu vingi, vitabu ambavyo vimeongeza idadi kubwa ya vitabu kwenye maktaba za Kiislam, na utafiti huu ambao uko mikononi mwetu ni ushahidi wa hayo, kila tunapomtaka Sheikh tubadilishe mihadhara yake katika maudhui mbalimbali muhimu anayoyatoa katika mimbari hukubali, pamoja na kubanwa kwake na wakati na majukumu aliyokuwa nayo hutujibu mara zote katika kila ambalo lina maslahi kwa jamii.

Maudhui haya ni miongoni mwa mihadhara ya Sheikh, ambaye kwa kawaida huzungumza na jamhuri pana katika matabaka tofauti ya watu, na yeye mwenyewe amesimamia na kurudia mara kwa mara katika kuyahakiki, na mwisho wake akatoa ruhusa yake ya kuchapishwa.

Maudhui haya yanatokana na hotuba yake aliyoitoa Qatwif, tarehe 2/1/1416 A.H. Maudhui haya yanahusiana na 'Nchi na Uraia, Haki na Wajibu Kwa Taifa.' Maudhui haya ni ushahidi uliopotea katika uwanja wa mazingatio ya Kiislamu, na ni moja ya maudhui yanayomuambatanisha mwanadamu Mwislamu na taifa lake na sehemu anayoishi kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine ni mahusiano yake na jamii yake, na hasa katika kipindi hiki kigumu, kipindi ambacho umepotea umoja wa Ummah wa Kiislam katika utandawazi wake, hali iliyopelekea kudhoofika kwa dola ambazo zimeimarisha mipaka yao inayotenganisha nchi zao, hali iliyopelekea kudhoofika maana ya utandawazi wa Taifa la Kiislamu.

Hivyo ikaonekana ni wajibu kutatua jambo hili na tatizo la uratibu wa mahusiano kati ya mwanadamu na taifa lake na nchi anamoishi ndani yake katika mipaka ya dola. Tunataraji utafiti huu wenye thamani wa Sheikh Hassan Saffar utatoa majibu kuhusu jambo hili, kama tunavyotarajia kufanikisha katika kuandaa mihadhara yake mingine ambayo hutatua matatizo na mambo muhimu tofauti ya ki-



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 5 7/31/2013 1:54:31 PM

jamii ili tuweze kuzichapisha hivi punde Inshaallah. – Walhamdulilahi Rabil-Alamina.

**Dhakir Aali Habil**
**Qatwifu,**
**15/Shaban/1416 A.H.**



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 6 7/31/2013 1:54:31 PM

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ

# UTANGULIZI

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuwekea mwanadamu matamanio na matakwa, na kutokana na matamanio na matakwa mwanadamu hupanua njia yake katika kuishi, matamanio haya yanahitaji maelekezo na kanuni, hivyo kuwako kwake (hayo matamanio) ni jambo muhimu kwa mwanadamu, kwa mfano, utashi wa mtu kujipenda mwenyewe, jambo hili ni muhimu katika maisha ya mwanadamu, kwa sababu ya kuwepo utashi huu mwanadamu anaweza kuihami nafsi yake, na kuutetea uhai wake, kama vile anavyojiletea maendeleo binafsi na mafanikio, kwa hivyo kuna ulazima wa utashi wa kujipenda mwenyewe uwepo kwenye maisha ya mwanadamu, lakini jambo hili linahitaji maelekezo na mwongozo na kanuni ili mwanadamu asivuke mipaka.

Mfano mwingine, ni matamanio ya kijinsia, ambapo kutokana na matamanio hayo ndiyo sababu ya kupatikana mwendelezo wa familia za watu na kubakia jamii ya mwanadamu, na haya nayo ni moja ya matamanio muhimu katika maisha ya mwanadamu lakini pia nayo yanahitaji maelekezo, uongofu na kanuni ili yabaki kwenye njia yake na lengo sahihi, na hali ni hiyo hiyo kwa matamanio mengine.

Na katika matamanio aliyowekewa mwanadamu ni utashi wa kupenda mji wake na nchi yake, na hili nalo liko katika kila nafsi ya mwanadamu, huwa anapenda kwao na anapenda mji wake, anapenda ardhi ambayo amezaliwa au amekulia humo na kulelewa, haya ni matamanio ya asili ya kila mtu kupenda mji wake, wanachuoni pia



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 7 7/31/2013 1:54:31 PM

wameliona jambo hili lipo kwa wanyama wengi, jambo hili ndilo ambalo humfanya mwanadamu kuendelea kuwepo katika dunia hii.

Imamu Ali (a.s.) anasema: "Miji imeimarishwa kwa sababu ya kupenda nchi."[1] Lau kama si utashi huu wa matamanio ya kupenda nchi kuwepo katika nafsi ya mwanadamu, katu miji isingejengwa na kupambwa, na wala mwanadamu asingeweza kuufikia ukamilifu wake wa kimaendeleo ambayo wanadamu wameyashuhudia na kuendelea kuyashuhudia siku hadi siku, na uendelezaji wa ardhi unaofanywa na mwanadamu katika ardhi utaendelea maadamu sifa hii ipo katika nafsi ya mwanadamu, na ambayo kutokana nayo tunaona kumiliki na kung'ang'ania kwa nguvu na kuliko wazi kwa mwanadamu kwa kushikamana na mji wake na nchi yake.

[1] *Biharul Anwar*, Muhammad Baqir al-Majlisiy, Juz. 75, Uk. 45.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 8 7/31/2013 1:54:31 PM

# NCHI NI NINI, NA URAIA NI NINI?

Maana ya nchi kama ilivyoelezwa na Ibn Mandhur katika kitabu chake '*Lisanul-A'rab'* ni kwamba: *'Watwan'* (nchi) ni nyumba unayoishi, nayo ni makazi ya mwanadamu na sehemu yake, wingi wake ni *Awtwan*. Na *Autwanul-Ghanam wal-Baqar* yaani malazi yao na sehemu wanazolala mbuzi au ng'ombe, '*Watwana bilmakan'* alikaa sehemu. Na *Awtwana*: amefanya kuwa nchi yake. Wanasema: *Awtwana fulan ardha kadha wa kadha*, maana yake ni ameifanya kuwa sehemu ya kuishi na maskani yake.[2]

Ama maana ya nchi kwa istilahi ya kisiasa ya sasa hivi wanakusudia 'Nchi' ni ile sehemu ambayo mtu huishi kwa muda mrefu au sehemu ambayo mtu ana maslahi nayo au kuna familia yake.[3] Na Uraia: ni sifa ya anayeishi kwenye nchi na kufaidika na haki za nchi na kutekeleza yaliyo wajibu ambayo yamewekwa kutokana na muambatano wake na nchi.[4] Na Qur'ani Tukufu, haikutumia neno *'Watwan'* lakini imetumia neno '*Balad.'*

Na katika Qur'ani kuna Sura inayoitwa *'Suratul Balad.'*, (Mji) ambayo ni sura ya 90 katika Msahafu Mtukufu. Mwenyezi Mungu anasema:

لَآ أُقْسِمُ بِهَٰذَا ٱلْبَلَدِ ﴿١﴾ وَأَنتَ حِلٌّۢ بِهَٰذَا ٱلْبَلَدِ ﴿٢﴾

**"Naapa kwa mji huu! Nawe unaukaa mji huu.**

**(al-Balad 90: 1-2)**.

[2] *Lisanul-Arab*, Ibn Mandhur, Juz. 13, Harfu ' Nuun' uk. 451.
[3] *Al-Qamusiy Siyasiy*, Ahmad Atwiyya, uk. 1268.
[4] *Al-Mausuatu Siyasiyya, al-Muassassatul-Arabiyya liddirasati wan-Nashri*, Juz. 6, uk.373.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 9 7/31/2013 1:54:31 PM

Na pia kwenye Qur'ani lipo neno *'Baldat* na *bilaad*.[5] Kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema:

بَلۡدَةٞ طَيِّبَةٞ وَرَبٌّ غَفُورٞ ١٥

**"Mji mzuri na Mola Mwenye maghufira."** **(as-Sabaa; 34:15)**.

Na pia amesema:

إِرَمَ ذَاتِ ٱلۡعِمَادِ ٧ ٱلَّتِي لَمۡ يُخۡلَقۡ مِثۡلُهَا فِي ٱلۡبِلَٰدِ ٨

**"Wa Irama wenye maguzo? Ambao haukuumbwa mfano wake katika miji?"** **(Qur'an 89: 7- 8).**

Kama vile ambavyo Qur'ani ilivyotumia neno *'Diyar'* Mwenyezi Mungu anasema:

أَلَمۡ تَرَ إِلَى ٱلۡمَلَإِ مِنۢ بَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ مِنۢ بَعۡدِ مُوسَىٰٓ إِذۡ قَالُواْ
لِنَبِيّٖ لَّهُمُ ٱبۡعَثۡ لَنَا مَلِكٗا نُّقَٰتِلۡ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِۖ قَالَ هَلۡ
عَسَيۡتُمۡ إِن كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلۡقِتَالُ أَلَّا تُقَٰتِلُواْۖ قَالُواْ وَمَا
لَنَآ أَلَّا نُقَٰتِلَ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَقَدۡ أُخۡرِجۡنَا مِن دِيَٰرِنَا

[5] *Al-Mu'jam al-Mufahras Lialfadhil Qur'an*, Muhammad Muad Abdul Baqi, uk. 133-134.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 10 7/31/2013 1:54:32 PM

وَأَبْنَآئِنَا ۖ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ ٱلْقِتَالُ تَوَلَّوْا۟ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌۢ بِٱلظَّـٰلِمِينَ ﴿٢٤٦﴾

**"Wakasema: Itakuwaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na hali tumetolewa nje ya majumba yetu na watoto wetu? Walipoandikiwa kupigana, wakageuka isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua madhalimu." (Qur'an, 2:246)**.

Na katika hadithi tukufu ambayo tunaweza tukaitolea ushahidi, hadithi ambayo ni mashuhuri inayosema:

حُبُّ الوَطَنِ مِنَ الإيمَانِ.

**"Kuipenda nchi ni sehemu ya imani."**[6]

Basi miongoni mwa mambo ya kiimani, ni mwanadamu kuupenda mji wake na nchi yake.

**Kuipenda nchi:**

**Tukiangalia na kuisoma historia ya mwanadamu ya mataifa mbalimbali na ya jamii, tutakuta uzalendo wake na adabu zake vimechukua nafasi kubwa iliyoelezea hali ya mataifa na jamii hizo kupenda mno nchi zao na miji yao, na kuambatana kwao na udongo (sehemu) waliokulia na kulelewa humo, Waarabu walipokuwa wakisafiri walikuwa wakibeba udongo wa ardhi yao na kuunusa udongo huo, na kuuweka kwenye maji wanayokunywa, na hata wanafalsafa wa Kiyunani walikuwa wanafanya hivyo hivyo, amesema mshairi:**

[6] *Safinatul- Bihar*, Sheikh Abbas Al-Qummiy, Juz. 2, uk. 668.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 11 7/31/2013 1:54:33 PM

"*Tunatembea kwa kutambua matembezi yetu,*
*kwa kuhifadhi chakula kwenye sehemu za kuhifadhia.*
*Na lazima katika safari yetu tuwe na fumba la mchanga,*
*tunalinywa kwa kupenda tulipozaliwa.*"[7]

Mwanadamu kupenda mji haitegemei sifa nzuri na yaliyomo ndani ya nchi, inawezekana baadhi ya nchi kiuchumi, kijiografia au hata uzuri wa kimaumbile zina sifa nyingi zaidi kuliko za nchi nyingine, na huenda nchi hii haina hadhi ikilinganishwa na nyingine, lakini nchi kama nchi ilivyo hupendwa na raia wake na huambatana nayo, na kuisifu kwa nyimbo, kama anavyosema mshairi:

"*Tulikuwa tumeipenda, na haikustahiki kupendwa,*
*yawezekana kitu kikapendwa wala hakina uzuri.*
*Kama ardhi isio na hewa nzuri wala maji,*
*lakini inapendwa kwa sababu ni nchi.*"[8]

Hata kama hali ya hewa ya nchi hii na upatikanaji wa maji si mzuri ikilinganishwa na nchi nyingine, au hata kama itakuwa ni mbaya zaidi kuliko nyingine, yatosha kupendwa na mwanadamu kwa sababu tu ni mahala alipozaliwa, na asili yake iliyokita mizizi ndani yake, kwa hivyo siku zote huwa katika hali ya mafungamano nayo pasi na kumiliki kwingine.

Ibn Abbas amesema: "Lau watu wangekinai kwenye riziki wazipatazo kama walivyokinai kwa nchi zao, asingelalamika mtu yeyote juu ya riziki." Na miongoni mwa misemo ya zamani ni: "Lau kama si kuipenda nchi, mji ungeharibika."[9] Na nchi hufungamana

[7] Ibn Abil Hadid, *Sharhu Nahjul Balaghah*, Juz. 4, uk. 477
[8] Ibn Abil Hadid, *Sharhu Nahjul Balaghah*, Juz. 4, uk. 477
[9] Kitabu kilichotangulia.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 12 7/31/2013 1:54:33 PM

katika nafsi ya mwanadamu na kumbukumbu za utoto wake na kipindi cha ujana, ambacho ni kipindi cha kumbukumbu thabiti na za maana, anasema Ibn Rumiy:

*"Nchi imependezeshwa kwa watu wake,*
*ni makazi ya vijana walipitisha (maisha) yao huko,*
*wakikumbuka nchi yao wanakumbuka zama za ujana,*
*na hapo hufarijika."*[10]

[10] Kitabu kilichotangulia.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 13 7/31/2013 1:54:33 PM

# KUFUKUZWA KATIKA NCHI NA SHERIA YA JIHAD

Mwanadamu kuishi katika nchi yake na kufurahia maisha ndani ya nchi alimozaliwa, hiyo ni haki yake ya kimaumbile, haihitaji kupatiwa na mtu mwingine. Mwenyezi Mungu huwakemea watawala makafiri ambao huwasababishia raia Waumini kuikimbia nchi yao, si kwa sababu yoyote, isipokuwa ni kutokana na imani yao na dini yao. Kwa kweli kutofautiana imani na dini si sababu ya kumnyima mtu haki yake ya kuishi kwenye nchi yake.

Kwa mfano watu wa Nabii Luti waliwatishia Waumini kuwatoa katika miji yao kama adhabu, kwa sababu tu wamemwamini Mwenyezi Mungu na kwenda kinyume na tabia mbovu zilizokuwa zikifanywa na waovu miongoni mwa watu wake, Mwenyezi Mungu anasema:

وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِۦٓ إِلَّآ أَن قَالُوٓاْ أَخْرِجُوهُم مِّن قَرْيَتِكُمْ ۖ إِنَّهُمْ أُنَاسٌ يَتَطَهَّرُونَ ﴿٨٢﴾

**"Na halikuwa jibu la watu wake isipokuwa kusema: Watoeni mjini mwenu, maana hao ni watu wanaojitakasa."**

**(al-A'araf 7:82)**.

Na pia Nabii Shuaibu (a.s.), watawala waovu walimtishia silaha na kumtoa kwenye mji wake kwa nguvu ikiwa hatofuata mila zao potofu:



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 14 7/31/2013 1:54:33 PM

۞ قَالَ ٱلۡمَلَأُ ٱلَّذِينَ ٱسۡتَكۡبَرُواْ مِن قَوۡمِهِۦ لَنُخۡرِجَنَّكَ يَٰشُعَيۡبُ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مَعَكَ مِن قَرۡيَتِنَآ أَوۡ لَتَعُودُنَّ فِي مِلَّتِنَاۚ قَالَ أَوَلَوۡ كُنَّا كَٰرِهِينَ ﴿٨٨﴾

**"Wakuu waliotakabari katika kaumu yake wakasema: Ewe Shuaib! Tutakutoa wewe na wale walioamini pamoja nawe katika mji wetu au mrejee katika mila yetu. Akasema: Je, ingawa tunaichukia?" (al-A'araf 7:88).**

Inaonekana kwamba hii ndio njia ya watawala madikteta na mafisadi namna wanavyoamiliana na Manabii na Waumini, Mwenyezi Mungu anasema:

وَقَالَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ لِرُسُلِهِمۡ لَنُخۡرِجَنَّكُم مِّنۡ أَرۡضِنَآ أَوۡ لَتَعُودُنَّ فِي مِلَّتِنَاۖ فَأَوۡحَىٰٓ إِلَيۡهِمۡ رَبُّهُمۡ لَنُهۡلِكَنَّ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿١٣﴾

**"Na wale ambao wamekufuru waliwaambia mitume wao: Tutawatoa katika ardhi yetu au mrudi kwenye mila yetu. Mola Wao akawapa wahyi: Hakika tutawaangamiza madhalimu." (al-Hijri; 14:13).**

Kutokana na dhulma hii, ndipo Uislamu unapotoa hukumu ya kupigana Jihadi, kwa ajili ya kutetea haki ya kimaumbile, haki ya kuishi katika nchi, na hapo Uislamu unawataka watangaze vita dhidi ya madikteta wanaowanyima raia wao neema ya kuishi katika nchi yao na majumba yao.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 15 7/31/2013 1:54:33 PM

Mwenyezi Mungu anasema:

قَالُوا۟ وَمَا لَنَآ أَلَّا نُقَـٰتِلَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَقَدْ أُخْرِجْنَا مِن
دِيَـٰرِنَا وَأَبْنَآئِنَا ۖ ﴿٢٤٦﴾

**"Wakasema: Itakuwaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na hali tumetolewa nje ya majumba yetu na watoto wetu?"** **(al-Baqarah; 2:246)**.

Na amesema tena:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَـٰتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا۟ ۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ
لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾ ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَـٰرِهِم بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّآ
أَن يَقُولُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم
بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَـٰجِدُ يُذْكَرُ
فِيهَا ٱسْمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا ۗ وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓ ۗ إِنَّ
ٱللَّهَ لَقَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

**"Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia. Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila tu kwa kuwa wanasema Mola Wetu ni Mwenyezi Mungu. Na lau Mwenyezi Mungu asingeliwakinga watu kwa watu, basi yangeliv-**



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 16 7/31/2013 1:54:34 PM

**unjwa mahekalu na makanisa na (sehemu) za kuswalia na misikiti ambayo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi. Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye enzi.”**

**(al-Hajj 22: 39-40).**

Aya hizi tukufu zilizomo katika Surat Hajj, ndizo Aya za mwanzo kuruhusu kupigana Jihadi katika Uislamu.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 17 7/31/2013 1:54:34 PM

# DINI NA KUIPENDA NCHI YAKO

Kuna mahusiano thabiti kati ya dini na kupenda nchi, kwa sababu dini halisi ni ile ambayo athari zake huakisi katika mahusiano ya mwanadamu na vitu vinavyomzunguka, kwa hivyo huyafanya mahusiano hayo kuwa thabiti na yenye nguvu, ndio maana ikawa kuipenda nchi ni sehemu ya imani, na ni dalili ya utekelezaji wa hadithi hii tukufu isemayo:

حُبُّ الوَطَنِ مِنَ الإيمَانِ.

**“Kuipenda nchi ni sehemu ya imani.”**[11]

Basi ni kwanini mwanadamu asiipende nchi yake na asiambatane nayo? Wakati mwili wake umekomaa kwa chakula chake na kwa kunywa maji yake, na kunusa hewa yake iliyo safi, hakika kinyume cha hayo ni uovu na wala sio uadilifu. Na wakati kitendo cha mtu kuambatana na nchi na kuipenda kina matokeo mazuri, Imamu Ali (a.s.) anasema:

مِنْ كَرَمِ المَرءِ حَنِينُهُ إلَى أوطَانِهِ

**“Katika heshima za mtu ni kupenda kwake nchi yake.”**[12]

Na wakati Mtume (s.a.w.w.) ilipomlazimu kuuhama mji wake wa Makkah, mahala alipozaliwa yeye, na kuhamia Madina, alionesha hisia zake kakamavu kuhusu mji wake, na akaonesha jinsi gani

[11] *Safinatul- Bihar*, Sheikh Abbas Al-Qummiy, Juz. 2, uk. 668.
[12] *Biharul-Anwar*, Al-Majlisiy, Juz.71, uk.264.

alivyoupenda mji, na maumivu yaliyomsibu kwa kuuacha, kama ilivyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas (r.a.) kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) wakati alipokuwa anatoka Makka alisimama katika soko la Haz-warah (soko la Makka) na akasema:

وَاللهِ إنَّكَ لَخَيرُ أرضِ اللهِ؛ وَأَحَبُّ أرضِ اللهِ إليَّ؛ وَلَولَا أهلُك أخرَجُونِي مِنكَ مَا خرَجتُ مِنكَ

**"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Hakika wewe ni ardhi ya Mwenyezi Mungu iliyo bora, na ni ardhi niipendayo zaidi, na lau kama si watu wako kunitoa (kunifukuza), nisingetoka kwako."[13]**

Warram ibn Abi Firasi al-Malikiy al-Ashtary ameeleza katika kitabu chake *'Tanbihil-khawatir Wanuzhatun-Nawaadhir'* kinachofahamika kama mkusanyiko wa Warram, katika mlango ulio na anwani isemayo: Shauku na mapenzi ya mji na kupumbazika na familia, ni kwamba "Abban ibn Said alifika kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), Mtume akasema: 'Ewe Abban, vipi umewaacha watu wa Makka?' Akasema: 'Nimewaacha wakiwa katika hali mbaya, nimeuwacha mti wa mkumbazi ukiwa umekauka, nimeiwacha ncha ikiwa imemalizika.' Basi Mtume (s.a.w.w.) akabubujikwa na machozi."

Na ilikuwa inasemwa kuwa: "Kumiliki kwako kwenye sehemu uliyozaliwa ni utukufu wa asili yako."[14]

Na pindi Imam Zainul-Abidina anapohadithia jihadi ya babu yake; Mtume (s.a.w.w.) na juhudi yake, na usumbufu alioupata katika maisha yake ni pale alipouhama mji wake na kuishi ugenini, anasema katika dua ya pili katika dua zilizo kwenye Sahifatus-Sajadiyyah:

[13] *Subulul-Hudaa Warrashad Fii Siyrati Khayril-Ibadi*, Imamu Muhammad ibn Yousuf Aswalihiy Ashamiy, Juz. 3, uk. 236.
[14] *Sharhu Nahjul Balaghah*, Inb al-Hadid, Juz. 4, uk. 38.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 19 7/31/2013 1:54:35 PM

وَهَاجَرَ إِلَى بِلاَدِ الْغُرْبَةِ وَمَحَلِّ النَّأيِ عَنْ مَوْطِنِ رَحْلِهِ ، وَمَوْضِعِ رِجْلِهِ
وَمَسْقَطِ رَأسِهِ وَمَأنَسِ نَفْسِهِ إِرَادَةً مِنْهُ لاعْزَازِ دِيْنِكَ ،

**"Na akahama kwenda mji wa ugenini na sehemu ya mbali kutoka mji wake, sehemu ya makazi yake, maangukio ya kichwa chake (alipozaliwa), na mahala pa maliwazo ya nafsi yake, kwa lengo la kuitia nguvu dini Yako."[15]**

Na pia katika dua yake katika kuwaombea Maswahaba wa Mtume (s.a.w.w.), akimuomba Mwenyezi Mungu awape thawabu na malipo kwa kuvumilia kwao tabu ya kuhama kutoka kwenye miji yao, anasema:

وَاشكُرْهُمْ عَلَى هَجْرِهِمْ فِيْكَ دِيَارَ قَوْمِهِمْ،

**"Na walipe kutokana na kuhama kwao miji ya watu wao kwa ajili yako."[16]**

Mmoja wa wanachuoni amezitolea ufafanuzi dua hizi mbili za Imam Zainul-Abidina (a.s.) kwa kusema: "Licha ya kwamba Mtume (s.a.w.w.) na Maswahaba wamehama kuelekea mji wa Madina ambao ni ngome ya Uislamu na makao makuu ya dola yake, lakinii Imam (a.s.) ameeleza ya kwamba ni mji wa upweke."[17]

Na pia imepokewa kuwa Mtume (s.a.w.w.) alipotoka mji wa Makka na kwenda Madina aligeuka na kuutazama mji wa Makka, akifikiria kwamba hatorejea tena wala hatouona tena baada ya hapo, aliingiwa na huzuni na kuanza kulia, Jibrili (a.s.) alimuendea na kumsomea aya ya Mwenyezi Mungu isemayo:

[15] *Sahifatu Sajadiya*, Dua Na2.
[16] *Sahifatu Sajadiya*, Dua ya 4.
[17] Sheikh Muhammad Mahdiy Shamsu Din, *Al-Ijtimai Siyasiy al-Islamiy*, uk. 145.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 20 7/31/2013 1:54:35 PM

إِنَّ ٱلَّذِى فَرَضَ عَلَيْكَ ٱلْقُرْءَانَ لَرَآدُّكَ إِلَىٰ مَعَادٍۚ قُل
رَّبِّىٓ أَعْلَمُ مَن جَآءَ بِٱلْهُدَىٰ وَمَنْ هُوَ فِى ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٨٥﴾

**"Hakika aliyekulazimisha Qur›ani, bila shaka atakurudisha mahali pa Marejeo. Sema: Mola Wangu Ndiye anayemjua zaidi mwenye kuja na uongofu na aliyemo katika upotofu ulio dhahiri."**

**(al-Qasas; 28: 85).**

Na inasemekana ya kwamba aya hii iliteremshwa baada ya kufika Juhfah wakati wa kuhama kwake, Mtume (s.a.w.w.) aliingiwa na shauku ya sehemu aliyozaliwa na walipozaliwa wazazi wake, na mahala palipo na makao matakatifu ya Nabii Ibrahim (a.s.) (al-Kaaba), basi Jibrili (a.s.) alimshukia na akamwambia: "Je, una shauku na mji wa Makka?" Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Ndio." Basi hapo akamteremshia aya hii.[18]

[18] *Ritadhu Salikin*, Sayyid Ali Khan al-Madaniy, Juz.1, uk.475.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 21 7/31/2013 1:54:35 PM

# MIPAKA YA NCHI

Maana ya nchi katika dhana ya mtu aliye Mwislamu iko katika aina tatu:

**Aina ya kwanza: - Uraia wa kiimani.**

Ummah wa Kiislamu ni Ummah mmoja, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

إِنَّ هَٰذِهِۦٓ أُمَّتُكُمۡ أُمَّةٗ وَٰحِدَةٗ وَأَنَا۠ رَبُّكُمۡ فَٱعۡبُدُونِ ﴿٩٢﴾

**"Hakika Ummah wenu huu ni Ummah mmoja, na mimi ni Mola Wenu kwa hivyo niabuduni.."** **(Al-Anbiyaa 21: 92)**.

Kwa hivyo nchi zote zilizoko katika mamlaka ya Waislamu, Waislamu wote wana haki ya kuishi humo, kwani ni sehemu ya ardhi yao. Na hapo zamani Waislamu walikuwa wakiishi katika mtazamo huo wa kiimani na kiakida juu ya nchi, kiasi ambacho kulikuwa hakuna tofauti za mitazamo ya kisiasa, wala mipaka ya kijiografia yenye kuwatenganisha, wala mipaka ya kimajimbo inayokwamisha harakati za Waislamu, Ilikuwa Mwislamu akitoka Kaskazini mwa Afrika akielekea Jakarta, Kusini mwa Asia bila ya kuwa na hati ya kusafiria, au viza ya kuingia, wala kuhitaji kubadilisha pesa.

Lakini leo hii dola ya Kiislamu imegawanyika na kuwa nchi Hamsini, hii ni kwa sababu tu ya kukengeuka na kuwa mbali na mafundisho ya Uislamu, na ni kwa sababu ya ujinga, na pia kufanyiwa njama na maadui. Mipaka iliyotengenezwa katika dola za Kiislamu,



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 22 7/31/2013 1:54:35 PM

imekuwa kikwazo kikubwa kinachozuia umoja wa Ummah huu na utengamano madhubuti wa kisiasa na kiuchumi.

Bali mipaka hiyo imekuwa ni mabomu yanayolipuka na kupelekea vita vikali na mapigano yanayopelekea umwagaji damu mara kwa mara. Kwa mfano, vita vilivyotokea karibuni kati ya Iraq na Iran, ambavyo vilidumu kwa muda wa miaka nane, kiasi cha kupelekea Waislamu zaidi ya milioni moja wa nchi hizo mbili kupoteza maisha. Zaidi ya hayo, hasara kubwa ya kiuchumi ilipatikana, hasara inayokadiriwa kufikia mabilioni ya fedha. Kisha kukatokea vita kati ya Iraq na Kuweit, vita vilivyouchanganya ulimwengu wa Kiarabu, na kuwarejesha nyuma kiuchumi kwa miaka mingi!

Kwa upande wa hasara za kiuchumi Waarabu walipata hasara kiasi cha dola bilioni 676, ambayo ni matokeo ya vita vya Ghuba vilivyotokea mwaka 1990 mpaka 1991. Na ilifikia hasara za kiuchumi kwa Iraq dola bilioni 240, wakati Kuweit ilipata hasara ya dola bilioni 237. Ama kuhusu hasara waliyoipata Waarabu kwa ujumla ni dola bilioni 91.[19] Na bado kuna matatizo mengi yenye kusumbua katika mipaka ya nchi za Kiarabu.

Tunaweza kusema kwa kila huzuni na uchungu kwamba maana ya nchi kwa mujibu wa imani na itikadi imebakia kuwa ni kumbukumbu njema katika historia yetu iliyopita, na kubakia kuwa ndoto tunayotarajia kutokea kwake wakati ujao, ndio maana ikawa kuna hisia kali na manung'uniko yenye nia ya kusonga mbele yanayochomoza katika nyoyo za Waislamu wenye mwamko miongoni mwao, hisia ambazo huwasukuma kwenye kiwango kiwezekanacho katika kuungana na kusaidiana licha ya kuwepo mipaka waliyowekewa na kulazimishwa nayo.

**Aina ya Pili:** Uraia wa kisiasa, ambapo kila mtu huishi katika nchi yake ambayo yeye ni raia wa nchi hiyo, ambapo maisha yake na

[19] Gazeti la *Safir* la Lebanon la tarehe 22|4|1993.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 23 7/31/2013 1:54:35 PM

mustakabali wake vinafungamana na nchi hiyo ambayo yeye ni raia, na kama Mwislamu anatamani nchi mbalimbali za dunia kuingizwa ndani ya ulimwengu wa Kiislamu ulio mmoja na mkubwa, hakika hilo halimaanishi kwamba yeye hatobeba majukumu yanayohusu nchi hiyo anamoishi ndani yake, na kufaidika na hali ya nchi hiyo na mazingira na kushirikiana pamoja na wananchi wengine kwa hali na mali. Hakika hayo yote ni mfano tosha na wa wazi kwa mujibu wa uhalisia wa maisha.

**Aina ya Tatu:** - **Nchi ya asili:** Ni ile nchi ambayo mtu amezaliwa humo na kulelewa, ikiwa ni katika mji au kijiji, ambapo kuna ada zenye kuamsha hisia za mwanadamu na ni sehemu aliyo na mapenzi nayo na yenye shauku kwake, kwani hata kama atachukua uraia wa nchi nyingine, bado hisia zake na mvuto wake utakuwa katika nchi hiyo ya asili.

Kwani tunaona raia anaweza kuishi sehemu yoyote katika sehemu za nchi kwa malengo ya kusoma au kufanya kazi au kwa sababu nyingine yoyote, lakini atabaki kutafuta fursa ili arudi katika mji wake au kijiji chake hata kama hakuna maendeleo yoyote au majengo mazuri ikilinganishwa na huko anakoishi.

Aina hizi tatu ni zenye kuingiliana, na kushikamana, na kuchagua moja kati ya aina hizi hakupingani na aina nyingine, bali ni kuleta ufanisi zaidi.

Yawezekana kwamba baadhi ya fikra zisizo na msingi zinaweza kupelekea kuonekana kwamba kuna tofauti na mikinzano katika aina hizi tatu, lakini kwa kila mwenye fikra sahihi na uoni mzuri, huona kwamba aina hizi tatu humfanya mwanadamu kuwa mwananchi mwema na mzalendo halisi.

Kama anavyosema mmoja wa wanafikra: "Hakika kushikamana sana (na nchi) haimaanishi kukataa kuwepo mshikamano mwengine mdogo usio wa kiasili. Huo ndio ukweli unaoshuhudiwa na maumbile



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 24 7/31/2013 1:54:35 PM

ya mwanadamu aliye na akili timamu. Kwa Mwislamu wa kweli, ambaye utambulisho wake wa kwanza ni Uislamu na nchi yenye eneo pana sana, hisia zake za kimaumbile humuonesha kwamba yeye pia ana mafungamano mengine madogo na yasio ya kiasili, mafungamano hayo hufuata baada ya mafungamano ya Kiislamu, na wala hakuna ukinzani wowote. Ummah wa Kiislamu ni kama mwili mmoja wenye viungo tofauti, lakini licha ya tofauti hii mwili hautoki katika umoja wake.

Maumbile ya kibinadamu yanashuhudia kwamba, mwanadamu anakuwa na mafungamano ya dhati juu ya jamaa zake na ndugu zake, pia na nchi yake na mahala alipozaliwa, na pia kwa wananchi wenzake ambao wanazungumza lugha moja na walio katika dini moja, na kisha kuwa na mafungamano na kila mwanadamu, ambao Mwenyezi Mungu amewaumba katika umbile sawasawa kutoka kwenye nafsi moja (Adam).

Maumbile ya mtu mwenye akili timamu yanashuhudia kwamba hakuna ukinzani wowote juu ya aina hizi tatu za mafungamano ya kinchi, hii ikiwa ni kama mfano wa ngazi, ambayo kwa kawaida kila kidato kimoja kinakitegemea kidato kingine, kwa hivyo mahusiano mema yatapatikana ikiwa hakutokuwa na ubaguzi na magomvi katika aina hizi tatu. Kwa kufanya hivi hakutokuwa na matatizo yoyote kwa kuwepo mafungamano ya kinchi katika hali hii, ikiwa tu asili ya mafungamano yapo kwa kuzingatia Uislamu.

Pindi mwanadamu anaporejea katika maumbile yake ya asili atagundua kwamba ana mapenzi maalumu ya kupenda pale alipozaliwa, na kujinasibisha vyema na nchi yake, kwa kuilinda, kuitetea na kuihudumia kwa moyo wake, na huku akiwa na mafungamano ya dhati juu ya nchi yake iliyo kubwa zaidi (Uislamu), ambayo iliweza kuleta ushindi na matarajio, kama ilivyothibiti katika historia…”[20]

[20] *Intimaul-Islamiy wal-Watwaniy wal-Qaumiy Takamul am Tanaqudh*, Dr. Muhammad Ammara, *Majallatul-Qafila*, Juz. 43, uk. 2.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 25 7/31/2013 1:54:35 PM

# WAJIBU WA RAIA MBELE YA TAIFA LAKE

**Kwanza: Kunyanyua neno la Mwenyezi Mungu katika nchi yako:** Inampasa mwanadamu kulingania dini ya Mwenyezi Mungu katika sehemu yote ya ardhi na katika ulimwengu wote, lakini katika nchi anayoishi ni bora zaidi na yeye ni mwenye uwezo mkubwa mno katika kutekeleza jambo hilo. Bila ya shaka ulinganiaji ni wajibu wa Mwislamu katika ulimwengu wote, lakini inampasa kuanza na wale walio karibu naye zaidi, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصْطَبِرْ عَلَيْهَا ۖ لَا نَسْـَٔلُكَ رِزْقًا ۖ نَّحْنُ نَرْزُقُكَ ۗ وَٱلْعَـٰقِبَةُ لِلتَّقْوَىٰ ﴿١٣٢﴾

**"Na uwaamrishe watu wako kuswali na uwe na subra nayo. Hatukuombi riziki. Sisi tunakuruzuku wewe. Na mwisho mwema ni wa mwenye takua."** **(Twaha; 20:132)**.

Na anasema:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ قُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا ﴿٦﴾

**"Enyi mlioamini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto.."** **(Tahrim 66:6)**.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 26 7/31/2013 1:54:36 PM

Na anasema:

وَأَنذِرۡ عَشِيرَتَكَ ٱلۡأَقۡرَبِينَ ﴿٢١٤﴾

**"Na waonye jamaa zako wakaribu."**

**(Shu'araa; 26:214)**.

Kwa hivyo ni wajibu kwa Mwislamu kuanza kunyanyua dini ya Mwenyezi Mungu katika nchi yake na mji wake, na kueneza humo kheri na mafanikio.

**Pili: Kuitetea nchi dhidi ya maadui:** Inampasa mwanadamu pindi nchi yake inaposhambuliwa na maadui awe tayari kubeba jukumu la kuihami na kuilinda mipaka yake, na kama hajaitetea nchi yake na mji wake, ni nani atakayeitetea! Hivi atawaita watu wengine waje waitetee na kuihami! Amirul Muuminina; Ali bin Abi Talib (a.s.) anawaambia wale waliozembea katika kuzilinda nyumba zao na nchi zao kwa kusema:

أَيَّ دَارٍ بَعدَ دَارِكُم تَمنَعُونَ

**"Ni nyumba ipi mtakayoitetea baada ya kujizuia kuitetea nyumba yenu?!"[21]**

Na pia amesema:

[21] *Nahjul-Balaghah*, Khutba Na. 39.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 27 7/31/2013 1:54:36 PM

فَواللهِ مَا غُزِيَ قَومٌ قَطٌّ فِي عُقرِ دَارِهِم إلاَّ ذَلُّوا.

**"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Watu hawakupigwa wakiwa majumbani mwao isipokuwa hudhalilika."[22]**

**Tatu: Kusaidiana na wanaoshirikiana na wewe katika nchi yako:** Hakuna mwanadamu miongoni mwenu anayeishi peke yake ndani ya nchi yake, bali kuna wale tunaoshirikiana nao katika kuishi katika nchi hii. Raha zetu ni zao na shida zao ni zetu, wakiwa ni wenye kuipenda nchi kama vile sisi tunavyoipenda, na kuisifu kama vile sisi tunavyoisifu, mafungamano yao na nchi ni kama mafungamano yetu. Hivi ni viunganishi vinavyotuunganisha kati yetu na wao, licha ya kwamba imani ndio kiunganishi kikubwa katika mafunganano yetu sote, lakini hata kama imani na itikadi zetu si moja, kule kuwa sisi sote tunashirikiana kuishi katika nchi moja, inatosha kuwepo mafungamano maalumu pamoja nao. Na yatosha kuwepo mafungamano kwa vile sote tunashirikiana katika ubinadamu, licha ya kuwepo utofauti wa dini na imani, kwani tunamuona Mtume (s.a.w.w.) pindi alipohamia Madina na kusimamisha dola ya Kiislamu huko, alisaini mkataba mashuhuri wa kihistoria unaojulikana kwa jina la 'Mkataba wa Madina.' Ni mkataba unaoeleza bayana juu ya kuwepo mahusiano mema kati ya Waislamu wao wenyewe, na kwa upande mwingine kati ya Waislamu na Mayahudi waliokuwa wakiishi huko, na miongoni mwa yalioandikwa humo ni kama yafuatayo:

Ibn Is'haq amesema: "Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliandika maandishi kati ya Ansari na Muhajirina, na kuwekeana mkataba pamoja na Mayahudi, na kutambua dini yao na mali zao, na akawekeana nao masharti:

[22] *Nahjul-Balaghah*, Khutba Na. 27.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 28 7/31/2013 1:54:36 PM

'Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Hii ni barua kutoka kwa Muhammad; Mtume wa Waumini na Waislamu wa kabila la Kureshi na wale wa Yathriba (Madina) na wanaowafuata na kuambatana nao na wakaungana nao katika jihadi, na wao kuwa ni Ummah mmoja tofauti na wengine...

'Na kwa hakika yeyote atakayetufuata miongoni mwa Mayahudi atakuwa ni mwenye kunusuriwa na kuamiliwa vyema, bila ya kudhulumiwa wala kukandamizwa...

'Na kwa hakika Mayahudi watatoa pamoja na Waumini maadamu tu wanashambuliwa. Na hakika Mayahudi wa Bani Awfi ni taifa moja na Waumini……

'Na kwa hakika Mayahudi wa ukoo wa Najjar wana haki sawa na Mayahudi wa ukoo wa Awfi, na Mayahudi wa ukoo wa Harith wana haki sawa na Mayahudi wa ukoo wa Awfi, na Mayahudi wa ukoo wa Saida wana haki sawa na Mayahudi wa ukoo wa Awfi, na Mayahudi wa ukoo wa Jusham wana haki sawa na Mayahudi wa ukoo wa Awfi, na Mayahudi wa ukoo wa Awsi wana haki sawa na Mayahudi wa ukoo wa Awfi, na Mayahudi wa ukoo wa Tha'laba wana haki sawa na Mayahudi wa ukoo wa Awfi, isipokuwa Yule mwenye kudhulumu na kufanya makosa, kwani huyo hatoiangamiza isipokuwa nafsi yake na watu wake.

'Kwa hakika Mayahudi wana pato lao na Waislamu wana pato lao, na hakika wao wanasaidiana dhidi ya yule atakayepinga mkataba huu, na ni juu yao kupeana nasaha, na ni jukumu lao kufanyiana wema, na sio dhambi, na si sawa mtu kumdhulumu mwenzake, na siku zote utetezi utakuwa kwa mdhulumiwa, na Mayahudi watatoa mali zao pamoja na Waumini pale ambapo watakuwa katika vita, na ndani ya Yathriba (Madina) patakuwa ni mahala pema kwa watu



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 29 7/31/2013 1:54:36 PM

waliosaini mkataba huu, na jirani atakuwa kama nafsi ya mtu, si mwenye kudhuriwa wala kudhulumiwa.'[23]

Dr. Walim Sulaiman Qalada, aliyekuwa wakili na naibu spika wa Misri amesema katika hotuba yake aliyoitoa zamani katika makao makuu ya umoja wa mawakili wa Kiarabu, kuhuhsu utafiti na ufundishaji wa kanuni huko jijini Cairo, hotuba hiyo baadaye ilikusanywa na kuwa kitabu kilichopewa jina '*Attasaamuhud-diniy wa tafaahumu bain al-mu'taqadat,*' na kuchapwa mwaka 1986, humo alisema kuhusiana na 'Mkataba wa Madina:

"Maandishi haya (Mkataba wa Madina), naamini kwamba hayatofautiani kabisa na maelezo yanayosema kwamba, kunakuwa na umoja wa kitaifa licha ya kuwepo dini mbalimbali."[24]

Na mwanachuoni wa zama hizi; Sheikh Muhamad Shamsud-Din amefanya utafiti juu mkataba huu (Mkataba wa Madina), utafiti wake umelenga katika maeneo ya mapokezi, matini, marejeo, maana na dalili, ndani ya kitabu chake kijulikanacho kwa jina la '*Fil-ijtima'is-Siyaasiyil-Islamiy*.'

Licha ya wao kuwa ni Mayahudi lakini Mtume (s.a.w.w.) amewekeana nao mkataba wa amani ya kitaifa ambao kila upande una haki ya kuutekeleza, ni kwa nini...? Ni kwa sababu wao wanashirikiana na Waislamu katika mji mmoja, Mtume (s.a.w.w.) anataka kuweka maisha ya ushirikiano katika mji wa Madina kwa lengo la kuzuia mizozo na khitilafu, kwa hivyo akawalazimisha wote kuukubali mkataba huo wa amani wa aina yake ili wote waweze kuishi kwa ushiriki katika mji wa Madina, kwa sababu ni mji wa Waislamu na wasiokuwa Waislamu…

Na katika mfano mwingine, tunakuta pia suala la ujirani na haki zake na kuwafanyia wema majirani, jambo ambalo kwa mujibu

[23] *Siyratun Nabawiya*, Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 115.
[24] *Attasaamuhud-diniy wa tafaahumu bain al-Mu'taqadat,* uk. 23.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 30 7/31/2013 1:54:37 PM

wa sheria ya Kiislamu halina mafungamano na imani, kwa maana kwamba, jirani ana haki zake juu yetu, sawa jirani huyo ni Mwislamu au si Mwislamu. Sio lazima jirani yetu awe na dini kama tunayoifuata sisi ili ithibitike kwamba ni jirani, bali hata kama jirani sio Mwislamu tunalazimishwa kumfanyia wema na kuwa na mahusiano mazuri naye, na kumpa haki zake zote zilizoko juu yetu.

Imepokewa kwamba mtumishi wa Ibn Abbas (r.a.) alichinja mbuzi, Ibn Abbas akamwambia: "Utakapomchuna anza kugawa kwa jirani yetu Myahudi." Kisha Ibn Abbas akayarudia maneno hayo, yule mtumishi akasema: "Ni mara ngapi unasema maneno haya?" Akasema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hakuacha kutuusia juu ya jirani mpaka tukahofia kwamba atamrithisha."

Kutokana na maelezo haya, inaonesha kwamba Ibn Abbas (r.a) alikuwa na jirani Myahudi na alikuwa akimpa zawadi kama anavyompa Mwislamu, ili kuchunga heshima na haki za ujirani, kwa maana hii ni kwamba Uislamu hautofautishi katika kutenda wema na kutekeleza haki za kijamii kati ya Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu, wote wako sawa kwa mtazamo wa Uislamu.[25]

Hata kama tukitofautiana juu ya dini na jirani yetu hilo halimzuwii yeye kupata haki zake za ujirani anazozipata jirani Mwislamu, kwa sababu wote wanashirikiana katika kuishi kwenye ardhi moja na ni majirani, uhusiano ambao unawajibisha wao kusaidiana, na kila mmoja kutekeleza haki za mwenzake, na kila ambapo mahusiano ya aina hii yanaposhamiri, ndipo wananchi watakapoweza kudumisha zaidi umoja wao wa kitaifa, na hapo ndipo watakapokuwa na nguvu ya kuijenga na kuitumikia nchi yao, kwani wananchi wa nchi moja mara nyingi matarajio yao na machungu yao juu ya nchi yao yanakuwa mamoja. Ndio maana tunamuona Imamu Ali bin Abu Talib (a.s.) anaumia kwa ajili ya mwanamke asiyekuwa Mwislamu kama anavyoumia kwa

[25] *Sharhu risalatul-huquq*, Hasanu al-Qabanjiy, Juz. 2, uk. 534.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 31 7/31/2013 1:54:37 PM

ajili ya mwanamke Mwislamu bila ya kubagua, hii ilitokea wakati ilipomfikia habari ya uvamizi uliofanywa na jeshi la Mu'awiyah katika kitongoji cha Ambari na kuwatendea uadui wakazi wake, alisema:

وَلَقَدْ بَلَغَنِي أَنَّ الرَّجُلَ مِنْهُمْ كَانَ يَدْخُلُ عَلَى الْمَرْأَةِ الْمُسْلِمَةِ، وَالْأُخْرَى الْمُعَاهَدَةِ، فَيَنْتَزِعُ حِجْلَهَا وَقُلْبَهَا وَقَلاَئِدَهَا، وَرِعَاثَهَا، ما تَمْتَنِعُ مِنْهُ إِلاَّ بِالْإِسْتِرْجَاعِ وَالْإِسْتِرْحَامِ

"Na habari zimenifikia kuwa mtu miongoni mwao huingia kwa mwanamke Mwislamu na mwanamke Dhimiy (mtu aliyekubali kuishi chini ya utawala wa dola ya Kiislamu kwa salama na amani) na anampora pambo la mguuni (kikuku), bangili, kidani chake, na shanga, na hamuwezi kumzuia ila kwa kusema: '**Kwa hakika Sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na sisi ni wenye kurejea Kwake**.' (Qur'an, 2:156), na kuomba kuhurumiwa."[26]

Imamu Ali (a.s.) anakumbuka machungu ya mwanamke Mwislamu sambamba na machungu ya mwanamke asiyekuwa Mwislamu, kwa sababu yeye (a.s.) anataka kubainisha kwamba kule wao kuishi katika ardhi moja na kutokewa na dhulma na uvamizi mmoja kutoka kwa jeshi la Mu'awiyah, imesababisha pia machungu kuwa mamoja, na pia hisia za Imamu (a.s.) juu yao ni moja. Kwa hivyo basi inatulazimu hisia zetu ziwe moja kwa wale wote tunaoshirikiana nao katika nchi moja, zikiwa katika misingi ya kusaidiana, ambapo kwayo hunyanyua heshima ya nchi zetu na miji yetu, kwani nchi ni ya wote, na maslahi ni ya wote na hatari huwasibu wote, kwani nchi ni kama jahazi moja ambalo likipatwa na hatari inakuwa ya wote na mafanikio pia ni ya wote.

[26] *Nahjul-Balaghah*, Khutba Na. 27.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 32 7/31/2013 1:54:37 PM

Kwa vile nchi ni ya wote, na heri na shari pia huwa ni za wote, hivyo kwa kuwa kuna hisia hizi za kushirikiana katika heri na shari, muda wote raia wanapaswa kushirikiana na kusaidiana ili kujikinga na hatari, na kufanya kazi kwa bidii ili kuleta ustawi mzuri na bora wa nchi yao. Na ni upumbavu tofauti za rai za watu wa nchi moja na tofauti za madhehebu au hata mitazamo ipelekee kugawanyika na magomvi ndani ya nchi moja. Kwa kweli hilo sio sahihi hata kidogo na ni khiyana, na ni kinyume cha dini na akili. Kwa hakika akili na dini inatutaka kusaidiane na kuzidisha juhudi kwa ajili ya maendeleo, kama pia vinavyotutaka kuwa pamoja na kuungana, kwa vile kuna sababu shirikishi, na hata kama kutakuwa hakuna imani na itikadi moja na inayokubalika na raia wote katika kila kipengele, kushirikiana katika ardhi moja na nchi moja kunalazimu kuwepo mahusiano mazuri na mema.

Na serikali zinazojali na zenye ukweli katika kuhakikisha maslahi ya wananchi wake na umoja wao, ndizo zinapaswa kuhakikisha unakuwepo mshikamano na umoja baina ya wananchi wake. Zihakikishe inakuwepo amani na utulivu ambao utaondoa tofauti za ndani ya nchi, ambao utapelekea heshima ya nchi na maendeleo yake. Imepokewa Hadithi isemayo: "Viongozi wema ni wale wanaowapatanisha waliotofautiana, na viongozi wabaya ni wale wanaowatenganisha walioshikamana."

**Nne: Mwanadamu kutenda kwa ajili ya maendeleo ya nchi yake na kunyanyua heshima yake:** Nchi hutukuka kutokana na watu wake, na huendelea kutokana na juhudi zao na kusaidiana kwao, pindi wananchi watakapochapa kazi kwa bidii na kutumia uwezo wao kiakili na juhudi zao za hali ya juu na kuitumikia vyema nchi yao, natija yake ni kuwepo maendeleo katika nchi na kuheshimika. Ama wananchi wakifanya upuuzi na uzembe, itapelekea nchi yao kuzorota na kudumaa na kutopiga hatua za kimaendeleo na ku-



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 33 7/31/2013 1:54:37 PM

poromoka katika kiwango cha kijamii na kitaifa, na kile cha kimataifa.

Jambo la muhimu kwa mwanadamu ni kujitahidi katika kufanya kazi kwa ajili ya kuiletea maendeleo nchi yake katika sekta mbalimbali. Basi mwenye elimu anapaswa kuitumia elimu yake kwa ajili ya kuihudumia nchi yake na raia wenzake, na pia mwenye uwezo wa kimali, atumie utajiri wake kwa ajili ya maendeleo ya nchi yake kwa kuanzisha miradi itakayotoa ajira kwa wananchi na kuwasaidia wale wasio na uwezo. Ama ikiwa mali itabakia katika mabenki bila ya kuendelezwa, natija yake ni kuwepo kwa hali mbaya ya uchumi na kurudi nyuma kimaendeleo. Kwa hivyo basi, sote kwa pamoja ni wajibu wetu kwa mtu mmoja mmoja na kwa makundi kufanya kazi kwa bidii na maarifa kwa kutumia ujuzi wetu ili kila mmoja achangie katika kuiletea nchi yetu maendeleo na heshima ya juu.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 34 7/31/2013 1:54:37 PM

# HAKI ZA RAIA

**Kwanza: Heshima:**

Pindi zikipatikana kwa mwanadamu sababu na vielelezo vya heshima na akahisi kwamba utukufu wake unaheshimiwa, hiyo humfanya ashikamane kwa nguvu zote na nchi yake na huzidisha hisia zake katika kujikita na kubakia kwenye nchi yake na kuwapenda wote kwa kule kujihisi kwamba kila mmoja anamuheshimu mwenzake. Qur'ani Tukufu inaelezea wale watu ambao wamepoteza heshima katika nchi zao na kutoweza kuupigania uhuru wao wa kimsingi katika nchi zao, watu hao wakawa na moja kati ya maamuzi mawili; ima kuishi katika hali ya udhalili, au kuihama nchi yao na kwenda kuishi ugenini ili kutafuta uhuru na heshima, na katika hali hii, maamuzi ya pili ndio sahihi kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

إِنَّ ٱلَّذِينَ تَوَفَّىٰهُمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ ظَالِمِيٓ أَنفُسِهِمۡ قَالُواْ فِيمَ كُنتُمۡۖ
قَالُواْ كُنَّا مُسۡتَضۡعَفِينَ فِي ٱلۡأَرۡضِۚ قَالُوٓاْ أَلَمۡ تَكُنۡ أَرۡضُ
ٱللَّهِ وَٰسِعَةٗ فَتُهَاجِرُواْ فِيهَاۚ فَأُوْلَٰٓئِكَ مَأۡوَىٰهُمۡ جَهَنَّمُۖ وَسَآءَتۡ
مَصِيرًا ٩٧

**"Hakika wale ambao Malaika wamewafisha hali ya kuwa wamezidhulumu nafsi zao, wataambiwa: Mlikuwa katika hali gani? Watasema: Tulikuwa wanyonge katika ardhi. wataambiwa: Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa pana mkahamia humo? Basi hao makazi yao ni Jahannam; nayo ni marejeo mabaya." (an-Nisa'a 4:97)**.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 35 7/31/2013 1:54:37 PM

Kwa hivyo, mwanadamu hatakiwi kukubali udhalili na kukandamizwa na kushushwa hadhi yake, na pindi anapoheshimiwa ndipo mapenzi na uzalendo kwa nchi yake unapozidi.

**Pili: Amani:**

Kila ambapo mwanadamu anahisi amani ya nafsi yake, mali yake na ya familia yake, ndipo anapozidisha mapenzi na kuwa karibu na kujiambatanisha zaidi na nchi yake, na anakuwa zaidi na zaidi ya hivyo, imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) akisema:

لاَ خَيرَ فِي الوَطَنِ إلاَّ مَعَ الأمنِ.

**"Hakuna heri katika nchi isipokuwa kukiwa na amani."**[27]

Imamu Ali (a.s.) anatilia mkazo juu ya hilo kwa kusema: "Nchi mbaya ni ile ambayo haina amani kwa raia."[28]

Ikiwa mwanadamu hahisi amani katika nchi yake atalazimika kuihama, hata kama ana mapenzi nayo, kwani kutokuwepo amani humkosesha neema ya utulivu aliyopewa mwanadamu.

Kwa nini Waislamu wa mwanzo walilazimika kuhamia Ethiopia? Ni kwa sababu walikosa amani katika mji wa Makka, kwani maudhi ya Makuraishi yalifikia kiwango kikubwa, hali iliyowapelekea wakimbilie Ethiopia, na kutokana na hali hiyo Mtume (s.a.w.w.) naye alilazimika kuuhama mji wa Makka baada ya kukosa amani ya nafsi yake.

[27] *Biharul-anwar*, al-Majlisiy, Juz. 74, uk. 58.
[28] *Mizanul-Hikmah*, Shahriy, Juz. 10, uk. 527.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 36 7/31/2013 1:54:37 PM

Hali hii ya kukosa amani katika nchi inajirudia kila wakati na sehemu tofauti, kwa vile mapambano kati ya haki na batili yanaendelea. Katika ulimwengu wetu huu wa leo tunaona watu wengi wakiishi katika shida na matatizo ya ukimbizi, hiyo ni kutokana na kukosekana amani na usalama wa nafsi zao, mali zao na jamaa zao, hali hiyo imesababishwa na dhulma ya watawala madikteta au fitina mbalimbali. Na jambo la kusikitisha zaidi ni kuona na kusoma takwimu za Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani la Umoja wa Mataifa, ya kwamba asilimia sitini ya wakimbizi ni Waislamu kwenye wakimbizi wanaofikia milioni kumi na nane.[29]

Hayo yote ni kwa sababu gani?!!! Ni kwa sababu ya dhulma na uadui na kukosekana kwa amani katika nchi ambazo kwa bahati mbaya zinaitwa nchi za Kiislamu, kama ambavyo Mwislamu amelazimika kukimbilia na kuishi katika nchi zisizo za Kiislamu, kwa lengo la kutafuta amani na utulivu wa nafsi yake pamoja na watu wake, ni msiba mkubwa ulioje ambao sisi Waislamu tunaishi ndani yake!!

Neema ya amani katika nchi ni neema iliyo kubwa sana, ni neema ambayo kila mtu ana wajibu wa kuilinda na kuihifadhi, na kila aliye Muumini wa kweli hana budi kumuelekea Mola Wake kwa kumuomba amani na utulivu katika nchi yake, kama tunavyomshuhudia Imamu Zaynul- Abidina katika dua aliyokuwa akiiomba karibu na alfajiri katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani:

**اللهم واعطني السعة في الرزق والأمن في الوطن.**

**"Ewe Mola wangu nikunjulie riziki na amani katika nchi."[30]**

---

[29] *Jaridatul-Hayat*, litolewalo London, 30/4/1993.
[30] *Biharul-Anwar*, al-Majlisy, Juz. 95, uk. 91



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 37 7/31/2013 1:54:37 PM

**Tatu: Kujitosheleza Kiuchumi:**

**Mwanadamu ana mahitaji mbalimbali katika maisha yake ya kila siku, na ipasavyo ni kupata mahitaji yake kikamilifu katika nchi yake ili aishi kwa utulivu, na kuweza kutoa juhudi zake na nguvu zake katika kuijenga na kuiendeleza nchi yake, lakini pindi anapoyakosa hayo katika nchi yake kutokana na sababu mbalimbali analazimika kuishi katika hali ya ufakiri na kuombaomba, au kuihama nchi yake ili kwenda kutafuta riziki ya kumwezesha kuishi na kupata mahitaji mengine ya kimaisha.**

Kwa hakika kuwepo nafasi za kazi kwa wananchi zitakazowawezesha kupata mahitaji yao ya kila siku katika nchi yao ni moja kati ya mambo yanayoleta furaha, kama Imam Zainul-Abidin Ali ibn Husein (a.s.) anavyosema:

من سعادة المرء أن يكون متجره في بلده.

**"Miongoni mwa furaha ya mwanadamu ni biashara yake kuwepo nchini mwake."[31]**

Na kwa hakika kuishi maisha ya ufakiri katika nchi yako kunaleta mashaka na machungu, kwani maisha ya namna hiyo yanafanana na maisha ya uchungu ambayo mtu huyaishi wakati anapokuwa ugenini, Imamu Ali (a.s.) anasema:

المقل غريب في بلدته.

[31] *Biharul-anwar*, al-Majlisy, Juz. 100, uk. 7.



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 38 7/31/2013 1:54:38 PM

**"Fakiri ni mgeni ndani ya nchi yake."**[32]

Na amesema tena a.s:

**الغنى في الغربة وطن والفقر في وطن غربة.**

**"Kuwa tajiri nje ya nchi ni sawa na kuwa nchini kwako (sehemu ya kuzaliwa), na kuwa fakiri katika nchi yako ni sawa na kuwa ugenini."**[33]

Pindi maisha ya mwanadamu yanapokuwa magumu katika nchi yake hulazimika kuishi kama kwamba ni mgeni, licha ya kwamba mtu huyo ni mwenyeji na mwananchi wa nchi hiyo, na kinyume chake ni kwamba mtu anayekuwa ugenini na kuwa na uwezo wa kujipatia mahitaji yake ya kimaisha, inakuwa nchi ile ya ugenini ni kama nchi yake ya kuzaliwa. Na leo tunashuhudia watu mbalimbali wenye uwezo mkubwa wa kufanya kazi na wenye vipaji vya kielimu, hulazimika kuzikimbia nchi zao na kuishi ugenini kwa lengo la kutafuta riziki na uwezo wa kiuchumi, watu hao ni kama watu wengine wanaopenda kuishi nchini mwao na wala hawapendi kutengana na ndugu zao, lakini shida zinawafanya wafanye hivyo!

Kutokana na hali hiyo, ndio maombi ya Nabii Ibrahim (a.s.) kuuombea mji Mtukufu wa Makka baada ya kumaliza kujenga nyumba tukufu (al-Kaaba) yalilenga kwenye mambo mawili: Amani na uwezo wa kimaisha kwa wakazi wa mji huo, kama Qur'ani Tukufu inavyomnukuu kwa kusema:

[32] *Nahjul-Balaghah*, Maneno ya hekam Na. 3
[33] *Nahjul-Balaghah*, Maneno ya hekam Na. 57



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 39 7/31/2013 1:54:38 PM

وَإِذۡ قَالَ إِبۡرَٰهِـۧمُ رَبِّ ٱجۡعَلۡ هَٰذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَٱرۡزُقۡ أَهۡلَهُۥ
مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ ﴿١٢٦﴾

**“Na aliposema Ibrahim: Ewe Mola wangu! Ufanye huu uwe mji wa amani na uwaruzuku wakazi wake matunda.”**

**(al-Baqarah 2:126)**.

**اللهم آمين والحمد لله ربِّ العالمين.**



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 40 7/31/2013 1:54:38 PM

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia

18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 42 7/31/2013 1:54:38 PM

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 45 7/31/2013 1:54:38 PM

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 46 7/31/2013 1:54:38 PM

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 47 7/31/2013 1:54:38 PM

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 48 7/31/2013 1:54:38 PM

166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 49 7/31/2013 1:54:38 PM

187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
196. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a.s.)
198. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
199. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
200. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi ya Kiislamu
201. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
202. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a.s.)
203. Uongozi wa kidini – Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 50 7/31/2013 1:54:38 PM

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba’Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n’amavuko by’ubushiya
4. Shiya na Hadithi



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 51 7/31/2013 1:54:38 PM

# MUHTASARI



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 52 7/31/2013 1:54:38 PM

# MUHTASARI



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 53 7/31/2013 1:54:38 PM

# MUHTASARI



11_Nchi na Uraia_31_July_2013.indd 54 7/31/2013 1:54:38 PM